

Kufanya Benki

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Benki ni mahali ambapo wewe unaweza kuweka pesa zako salama.

Akaunti ya Benki ni nini?

Akaunti ya Benki ni mahali unapoweka pesa zako katika benki. Itakuwa kwa jina lako. Wakati unapoweka pesa kwenye akaunti inaitwa Kuweka (deposit). Wakati unapochukua pesa zako kutoka akaunti yako inaitwa Kutoa (withdrawal).

Benki hufanya kazi vipi?

Benki yako hurekodipesa unazozitokea (kuweka ndani) na kutoa (kutoa nje). Mabaki yako kwenye benki ni pesa taslim ambazo unazo kwenye akaunti wakati huo. Wakati unapoifungua akaunti kwenye benki utapatiwa debit kadi na Nambari ya Kibinafsi ya Kujitambulisha (PIN).

Debit kadi ni nini?

Debit kadi ni kadi ya plastiki inayotumiwa kutoa pesa kutoka akaunti ya benki, au kulipia bidhaa na huduma. Imeshikanishwa na akaunti ya benki yako na inatumia pesa zako pekee.

PIN ni nini?

Hii ni nambari za kibinafsi unayotumia kuweza kufikia akaunti yako ya benki.

Jinsi ya kufikia pesa zako?

Utahitaji debit kadi yako na PIN yako ili kutoa pesa zako kutoka kwenye akaunti yako.

Automatic Teller Machine: ATM ni mashine inayowezesha wateja wa benki kupata pesa zao kutoka akaunti zao bila kuenda kwenye tawi.

Electronic Funds Transfer at Point Of Sale: EFTPOS ni njia unayoweza kulipia bidhaa au huduma bila kuhitaji kubeba pesa.

Kumbuka:

- ▶ Kufanya benki ni wakati unapoweka pesa zako kwenye benki, umoja wa kusadiki au ujenzi wa jamii.
- ▶ PIN ni nambari ya kibinafsi unayoitumia kufikia akaunti ya benki yako.
- ▶ Usimwambia mtu yeyote PIN yako.
- ▶ Usiweke PIN yako pamoja na kadi yako ya benki.

Kwa maelezo zaidi kuhusu akaunti ya benki yako na ada, unaweza kuipigia benki au kutembelea tuvuti ya benki yako.



Liza anapata kugharamika kwa ada za benki

Pale Jumatatu Liza anahitaji pesa kununua tikiti ya gari la moshi ili kuhudhuria darasa la Kiiingereza ili atoe nje (atoe) \$20 kutoka ATM katika Benki ya Commonwealth ambapo anaweka pesa zake. Pale Jumatane alihitaji kununua kijitabu cha masomo yake alitoaili atoe \$20 kutoka ATM ya Westpac iliyopo nje ya duka la vitabu. Jumatano anapoenda kwenye sinema na kutoa \$30 kutoka kwenye ATM ya benki ya ANZ ATM katika sinema.

Liza anajua pesa zake za Centrelink zinatakiwa kuwa kwenye akaunti ya benki pale Alhamisi. Yeye huenda kwa ATM ya Benki ya Commonwealth iliyopo katika maduka yaliyomo kwenye eneo lake ili kuhakikisha kuwa pesa zake zimewekwa kwenye akaunti yake. Liza alishangaa wakati anapokuwa na pesa kidogo kwenye akaunti yake kuliko alivyotarajia. Anapata wasiwasi kwa sababu anahitaji pesa za kulipa kodi yake ya nyumba na kununua chakula.

Liza haelewi bona hana pesa kwenye akaunti yake na anashangaa kama ATM imekosea makosa na kumuambia akaunti ya makosa. Kwa hivyo aliitembelea benki na kuongea na mtu ambaye anafanya kazi pale anayetitwa Sandeep.

Sandeep alimuelezea Liza kuwa kiasi cha pesa kilicho kwenye akaunti yake ni sawa. Pia aliweza kumuelezea Liza kuwa anapesa chache kwa sababu ameshalipia ada ya kuchukua pesa nje kutoka kwa ATM aliyoitumia. Sandeep alimuelezea Liza kuwa lazima alipe ada wakati anapotumia ATM ambayo si mali ya benki yake na pia wakati anapochukua pesa kutoka kwenye ATM mara nyingi zaidi kwenye juma.

Sandeep alipendekeza kuwa Liza afanye Taarifa ya Gharama ili kupata kugundua pesa ngapi anahitaji kwenye juma. Halafu alipendekeza kuwa Liza azitoe pesa kutoka kwenye ATM kupitia shughuli moja. Hii ni mojawapo ya njia ya kuzuia kulipishwa kwa ajili ya shughuli mingi.

This page has been intentionally left blank.